# DIOCESE OF IRINGA

## SAN GIOVANNI PAOLO SECONDO SEC. SCHOOL-KITANEWA

Kitanewa Parish-Idodi. 3kms from the Main Road to Ruaha National Park (Eastward)
P.O BOX 1220, IRINGA. Mobile: 0769755214/0719515012/0758465497.
Email: sgpsecondo@gmail.com

***FOMU YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA-2026***

Jumuiya ya Shule ya Sekondari ya San Giovanni Paolo Secondo inayo furaha kukuarifu rasmi kuwa mtoto wako………………………………………………………………............................ amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii. Shule ipo katika Wilaya ya Iringa, Kata ya Idodi kijiji cha Mapogoro/Kitanewa. Shule inamilikiwa na Katoliki Jimbo la Iringa.

Ada ya shule ni sh. 1,350,000/= na inaweza kulipwa kwa awamu tatu (3) kwa mwaka. Ilipwe kwenye Benki ya **CRDB** akaunti namba: **0150601109100**, jina la Akaunti **SAN GIOVANNI PAOLO SECONDO** na mwanafunzi aje na bank slip shuleni kwa uthibitisho.

**MCHANGANUO YA MALIPO YA ADA KWA MWAKA.**

| AWAMU YA KWANZA | AWAMU YA PILI | AWAMU YA TATU |
|---|---|---|
| JANUARI | APRILI | JULAI |
| 450,000/ | 450,000/ | 450,000/ |

1. **SARE ZA SHULE**
   I. Suruali ya kijani na shati nyeupe mikono mifupi (suruali 2, shati 2- wavulana) na sketi ya kijani ndefu na shati la mikono mifupi –wasichana (sketi 2, shati 2), vyote vinapatikana hapa shuleni kwa gharama nafuu kabisa. Shati shilingi 13,000/=, suruali/sketi shilingi 20,000/=, kila moja.
   II. Viatu vya ngozi vyeusi vyenye kufunga na kamba.
   III. Soksi nyeupe jozi/pea mbili (zinapatikana hapa shuleni-sh.1000/=)
   IV. Sweta la blue ya kuiva (linapatikana shuleni kwa gharama ya shilingi 10,000/=
   V. Nguo za kushindia/shamba dress/kuvaa wakati wa shughuli za nje ni sketi nyeusi na T-shirt kwa wasichana, na suruali nyeusi na T-shirt kwa wavulana kwa gharama ya shilingi @ 15000 (jumla ni sh. 35000/=)
   VI. Nguo za michezo ni track suit nyeusi (wavulana na wasichana) zinapatikana shule kwa gharama ya sh. 25000/=
   VII. Viatu vya michezo (raba)
   VIII. Picha nne (4) passport size akiwa amevaa shati nyeupe mikono mifupi.
   IX. Kamusi ya Kiingereza (zinapatikana shuleni kwa gharama ya shilingi Elfu ishirini tu 20,000)

**MUHIMU**: Kwa kuwa wanafunzi wengi wanashona mishono tofauti na isiyofaa, tunashauri sana sare zote zishonwe shuleni.

**MAHITAJI MENGINE YA MUHIMU**

I. Ream paper 2 kwa mwaka (zinapatikana shuleni kwa gharama ya sh. 15,000/=@ 1)
II. Godoro la futi tatu (linapatikana shuleni kwa gharama ya sh. 35,000/).
III. Shuka pea mbili (moja rangi ya pinki, nyingine rangi ya blue bahari
IV. Taulo la kuogea
V. Chandarua moja rangi ya blue.
VI. Sahani, kijiko, kikombe, bakuli, ndala na toilet papers/karatasi ya chooni kwa ajili ya matumizi binafsi
VII. Ndoo ndogo ya lita 10
VIII. Sanitarian pads 6 (pedi) kwa wasichana (zinapatikana shuleni)
IX. Sabuni za kuogea na kufulia (za kutosha)
X. Kwanja moja, jembe, na mpini wake, mfagio (soft bloom ndefu) mmoja, squeezer 1 na fagio la nje 1
XI. Kaunta book 12, kalamu za kutosha, rula moja na mathematical set (vyote vinapatikana shuleni, tunashauri mtoto atumie Kaunta Book kubwa ili kusiwe na usumbufu wa kubadirisha mara kwa mara).
XII. Kiwi, brash ya viatu, mswaki na dawa ya meno, Sabuni na nguo za ndani za kutosha (vinapatikana shuleni).
XIII. Picha 3 za ndugu, wazazi/walezi watakaoruhusiwa kumtembelea mwanafunzi shuleni.
XIV. Sanduku la chuma kwa ajili ya kutunzia vifaa vyake
XV. Nakala ya cheti cha kuzaliwa.
XVI. Nakala ya Result slip darasa la Saba.
XVII. Spring file moja kwa ajili ya kutunzia mitihani.
XVIII. Mwanafunzi anapaswa kuwa na pesa ya matumizi pindi awapo shuleni na pesa hiyo ilipwe kupitia lipa namba ya shule(58171260 jina SAN GIOVANNI PAOLO SECONDO) **.**

**MUHIMU**: ***MZAZI ALIPE FEDHA YA TAHADHARI (CAUTION MONEY). Kiasi cha sh***. Elfu arobaini (40,000/= tu kwa mwaka. Fedha hiyo ilipwe kwa lipa namba (voda lipa namba-58171260, San GIOVANNI PAOLO SECONDO).

ZINGATIA: Michango yote ilipwe kupitia lipa namba ya shule na ada ilipwe kupitia akaunti namba ya benki, ambazo zimeainishwa hapo juu na si vinginevyo.

## 2. MAKOSA YANAYOSABABISHA MWANAFUNZI AFUKUZWE SHULE

i. Wizi na makosa ya jinai
ii. Kutohudhuria masomo kwa muda wa siku 90 bila sababu maalum/taarifa.
iii. Kugoma/kuhamasisha mgomo.
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, kwa walimu, walezi au jamii kwa ujumla.
v. Kupigana, kumpiga mwalimu au mtu yoyote.

vi. Kufuga ndevu au kuvuta sigara.
vii. Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa.
viii. Kupata ujauzito/kutoa mimba kwa wasichana.
ix. Kukutwa kwenye nyumba za kulala wageni na kumbi za starehe.
x. Kudharau Bendera/ wimbo wa Taifa.
xi. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu nk.
xii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shuleni.
xiii. Kuharibu mali ya shule kwa makusudi.
xiv. Kukaribisha wageni shuleni bila ruhusa.
xv. Kuingia maabara bila kibari cha mwalimu.
xvi. Utoro wa kudumu.

**MUHIMU:**

a) Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo za nyumbani.

b) Mwanafunzi haruhusiwi kufuga wala kusuka nywele au kunyoa mitindo isiyo na staha kama vile denge nk.

c) Mzazi/mlezi pamoja na mwanafunzi zingatia kwa makini sheria namba XII, kwani kukiuka sheria hiyo itapelekea kulipa faini ya shilingi laki mbili (200,000/= au kufukuzwa shule au vyote viwili kwa pamoja.

**<u>SHERIA NA KANUNI ZA SHULE</u>**

i. Ni lazima kusimama na kusalimia mwalimu, mfanyakazi au mtu yoyote anayekuzidi umri anapopita au anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano
ii. Mwanafunzi haruhusiwi kutumia lugha mbaya wakati wote kwa mwanafunzi mwenzake, mwalimu ndani na nje ya shule
iii. Ni lazima kuheshimu bendera ya nchi na serikali, picha za viongozi wa serikali, Nembo ya Taifa, Wimbo wa Taifa na Fedha ya Taifa
iv. Ni lazima mwanafunzi kuheshimu ofisi za shule, mali za shule na za wengine, ukumbi wa mikutano (Conference Hall), na mahali pa kulia chakula (Dining Hall).
v. Ni lazima mwanafunzi kusimama anapoulizwa au kujibu swali.
vi. Mwanafunzi ni lazima kukaa kimya wakati wote awapo darasani, chumba cha chakula au muda awapo chumbani (wakati wa kulala).
vii. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuondoka shuleni bila kibali maalum cha mwalimu
viii. Ni marufuku kujisaidia hovyo, kutupa taka hovyo, kukata miti au maua
ix. Ni marufuku mwanafunzi kuonekana au kwenda kwenye nyumba za walimu au watumishi bila kibali maalum kitakachotolewa na mkuu wa shule.

*"Ni matumaini yetu kuwa daima utatii Sheria, Taratibu na Kanuni za shule ili uwe mwanafunzi bora"*.

*KARIBU SANA SHULENI SAN GIOVANNI PAOLO SECONDO KWA ELIMU BORA.*

**FOMU HII IJAZWE NA MGANGA MKUU WA HOSPITALI YA SERIKALI**

Mwanafunzi aje nayo shuleni na kuikabidhi kwa Mkuu wa shule

Mimi (jina la Mganga)...........................................................................................................

Ninathibitisha kuwa mwanafunzi huyu (jina la mwanafunzi) ..........................................................

Amepimwa na mimi kikamilifu na kuonekana kuwa anayo/hana afya nzuri kwa mujibu wa taarifa zifuatazo: -

**A. HALI YA MWILI**

1. Mapigo ya moyo.........................................................................................
2. Damu (Haemoglobin)...................................................................................
3. Kundi la damu (blood group) .........................................................................
4. Mkojo.........................................................................................................
5. Haja kubwa..................................................................................................
6. Macho.........................................................................................................
7. Masikio.......................................................................................................

NB: weka maoni yako kuhusu kile kilichotajwa

**B. MAGONJWA**

Amewahi/hajawahi au hana magonjwa yafuatayo,

1. Kifua Kikuu (TB)..........................................................................................
2. Kifafa (Epilepsy)..........................................................................................
3. Shinikizo la damu (BP)..................................................................................
4. Magonjwa ya tumbo.......................................................................................
5. Seli mundu (sickle Cell) ..................................................................................
6. Magonjwa ya zinaa (taja aina) .........................................................................
7. Ugonjwa wa akili...........................................................................................
8. Ugonjwa mwingine nje ya orodha hapo juu.......................................................

NB: Maoni ya daktari...............................................................................................

....................................................

Sahihi na muhuri wa Daktari

................................................

Mkuu wa shule